# Gekul awaagiza wakurugenzi halmashauri kutenga fedha za mifugo

**Na Mbaraka Kambona, Kilimanjaro**

■■NAIBU Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Pauline Gekul amewataka Wakurugenzi wa Halmashauri zote nchini kutekeleza Waraka wa mwaka 2002 ambao unawataka kutenga asilimia 15 ya mapato yanayotokana na shughuli za sekta ya mifugo na uvuvi na kuzirejesha kwenye sekta hizo ili kuboresha shughuli zake.

Gekul alitoa agizo hilo alipokuwa akiongea na viongozi wa Wilaya ya Mwanga, Mkoani Kilimanjaro alipotembelea kukagua shughuli za Sekta ya mifugo na uvuvi zinazotekelezwa Wilayani humo.

Kwa mujibu wa Gekul, mwaka 2002 Serikali imetoa waraka ambao unaelekeza kuwa Halmashauri zote nchini zihakikishe kuwa mapato yanayopatikana kutokana na shughuli za sekta ya mifugo na uvuvi itengwe asilimia 15 na zirudishwe kwa sekta hizo ili kuboresha huduma kwa mifugo ikiwemo ukarabati wa majosho, minada na kununua chanjo za mifugo.

"Wakurugenzi rejeeni huo waraka ambao unadumu mpaka mwaka 2025 ili mtekeleze kama ulivyoagiza na tukifanya hivyo itasaidia kuboresha huduma za mifugo yetu na tupate mazao bora yanayotokana na mifugo hiyo," alisema Gekul.

Aliendelea kusema kuwa miundombinu mingi ya kuhudumia mifugo imechoka akitolea mfano minada ya kuuza ng'ombe kuwa mingi haina uzio, mifugo inauzwa katika maeneo ya wazi jambo ambalo linachangia upotevu wa mapato ya Halmashauri.

"Najua katika Halmashauri zetu mara nyingi fedha huwa hazitoshi lakini ni muhimu kujenga nidhamu ya matumizi ya fedha na tukifanya hivyo itakuwa rahisi kutenga hizo pesa ili kuboresha sekta za mifugo na uvuvi, hivyo naagiza baada ya kutoka hapa tukatekeleze hilo," alisisitiza Gekul.

Aidha, Waziri Gekul alisema kuwa muelekeo wa Serikali kwa sasa ni kuhakikisha majosho yanaboreshwa, minada inakarabatiwa na chanjo zinapatikana kwa urahisi ili wananchi wasihangaike kupata huduma kwa ajili ya mifugo yao.

Pia, aliwataka maafisa mifugo kuhakikisha wanasimamia vyema ukusanyaji wa maduhuli ya serikali ili kuzuia upotevu wa mapato kwani makusanyo yakiwa mazuri na huduma za mifugo zitaboreshwa.



Mkurugenzi, Idara ya Uvuvi, Wizara ya Mifugo na Uvuvi, Magese Bulayi (wapili kushoto) akitoa maelezo kwa Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Pauline Gekul (katikati) kuhusu moja ya nyavu inayotumiwa na wavuvi wanaofanya shughuli zao katika bwawa la Nyumba ya Mungu lililopo Wilayani Mwanga, Mkoani Kilimanjaro. Waziri Gekul alikwenda katika Mwalo wa bwawa hilo kukagua shughuli zinazoendelea hapo Desemba 23, 2020. Wa kwanza kulia ni Mbunge wa Simanjiro, Christopher Ole Sendeka. (Na Mpigapicha Wetu)

## Diwani Kata ya Matema ampongeza Rais Magufuli

**Na Julius konala, Kyela**

■■DIWANI wa Kata ya Matema katika Wilaya ya Kyela mkoani Mbeya Antony Mwamgunda, amempongeza na kumshukuru Rais Dkt.John Magufuli kwa jitihada zake za kuboresha miundombinu ya barabara kwa kiwango cha lami na umeme kutoka njia panda ya Ipinda hadi kijiji cha Matema Beach wilayani humo.

Mwamgunda alitoa pongezi hizo mwishoni mwa wiki wakati alipokuwa akizungumza na gazeti hili wilayani humo kwa lengo la kueleza mikakati mbalimbali ya maendeleo ya kata hiyo.

Alisema kuwa tangu Serikali ya Awamu ya Tano inayoongozwa na Dkt.Magufuli iboreshe miundombinu hiyo ya barabara imechangia kukuza uchumi wa kata ya Matema.

Alifafanua kuwa kutekelezwa kwa miradi hiyo ya barabara na umeme imechangia kuwavutia wawekezaji wa hoteli na nyumba za kulala wageni pamoja na watalii toka ndani na nje ya Nchi na kuipatia serikali fedha za kigeni.

Aidha Mwamgunda ameiomba Serikali kuangalia uwezekano wa

Scanned with CamScanner

# Gekul directs councils to plough back 15 pc of revenue to livestock services

By Guardian Correspondent, Moshi

Livestock and Fisheries deputy minister, Pauline Gekul has directed all local council executive directors in the country to implement the 2002 Government Circular that called on them to plough back 15 per cent of their revenue collections from the livestock and fisheries sectors to improve them.

She issued the directive on Wednesday this week when she addressing Mwanga District officials in Kilimanjaro Region during her visit to inspect livestock and fisheries activities.

Gekul said in 2002 the government issued the Circular, saying the money ploughed was to be used to improve livestock services including refurbishing of cattle dips, auctions management and purchase of animals' vaccines.

"Refer back to the 2002 Circular that is in force until 2025, as that will enable the improvement of livestock services in order to reap quality products from the livestock," she told the district directors.

She said many infrastructure serving the livestock were worn out and gave an example of cattle auctions, many which were conducted in open areas without any fencing, the situation contributing to loss of local councils' revenues.

Gekul said the government's goals as for now was to ensure cattle dips are refurbished, auctions infrastructure are revamped and vaccines are available.

She also called on livestock officers to supervise well government levies to plug revenue losses, saying good revenues means better livestock services.

Scanned with CamScanner

# NHIF yalipa bilioni 4.4/- kwa watoa huduma

Na Alexander Sanga, Mwanza

MFUKO wa Taifa wa Bima ya Afya (NHIF), tawi la Mwanza umelipa madai ya Sh bilioni 4.4 kwa watoa huduma za afya mkoani Mwanza.

Meneja wa NHIF Mwanza, Jarlath Mushashu alisema katika kipindi cha Julai-Novemba mwaka huu wamelipa Sh bilioni 4 kwa watoa huduma 390 waliosajiliwa mkoani hapa.

Mushashu alisema wataendelea kulipa madai ya watoa huduma na kutengeneza kadi za wanachama. Kwa mujibu wa meneja huyo, Mkoa wa Mwanza una zaidi ya vituo 590 vya kutolea huduma, lakini vilivyosajiliwa na kutambulika ni vituo 390.

"Ndani ya mwezi Julai hadi Novemba mwaka huu, tumesajili vituo vipya 12 na zaidi ya vituo 100 vimeboresha mikataba yao," alisema.

Mkurugenzi Mkuu wa NHIF, Bernard Konga alisema mfuko wao upo katika mpango wa kuhakikisha unaongeza wanachama wapya na kwamba, wataendelea kuhakikisha madai ya wanachama wanalipwa.

"Tumepata malalamiko kuwa tunachelewa kulipa madai; kama mfuko tumeanzisha utaratibu wa kila kituo kuwa na uwezo wa mwanachama wetu kuwasilisha madai yake siku hiyo hiyo," alisema Konga.

Kaimu Mganga Mkuu wa Mkoa wa Mwanza, Dk Elias Misana, alisema mkutano huo na watoaji huduma utasaidia kutatua changamoto zinazowakabili watoa huduma.



Mkurugenzi, Idara ya Uvuvi, Wizara ya Mifugo na Uvuvi, Magese Bulayi (wapili kushoto) akitoa maelezo kwa Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Pauline Gekul (katikati) kuhusu moja ya nyavu zinazotumiwa na wavuvi wanaofanya shughuli zao katika bwawa la Nyumba ya Mungu lililopo Wilayani Mwanga, Mkoani Kilimanjaro. Waziri Gekul alikuwa katika mwalo wa bwawa hilo kukagua shughuli zinazoendelea hivi karibuni. Wa kwanza kulia ni Mbunge wa Simanjiro, Christopher Ole Sendeka (Na Mpigapicha Wetu).

# Mwanza watekeleza agizo la Majaliwa kuhusu madarasa

Na Nashon Kennedy, Mwanza

MKOA wa Mwanza umetekeleza agizo la Waziri Mkuu Kassim Majaliwa kuzitaka halmashauri nchini kuhakikisha ujenzi wa vyumba vya madarasa unakamilika ifikapo Februari 28 mwakani ili kuwezesha wanafunzi waliofaulu na kuchaguliwa kujiunga na kidato cha kwanza, kuanza masomo.

Kaimu Ofisa Elimu wa Mkoa wa Mwanza, Sheja Josephat, alibainisha hayo wakati akiwasilisha taarifa ya maendeleo ya elimu ya Mkoa wa Mwanza katika kikao cha Kamati ya Ushauri ya Mkoa (RCC).

Alisema Mkoa wa Mwanza umepokea Sh bilioni 2.15 katika Mwaka wa Fedha 2019/20 kwa ajili ya ujenzi wa vyumba vya madarasa na matundu ya vyoo kwa shule za msingi na sekondari.

Alisema kati ya fedha hizo Sh 1,125,000,000 zilitumika kukamilisha ujenzi wa vyumba vya madarasa katika shule za sekondari. "Maboma yote yamekamilika na tayari yanatumika," alisema.

Alisema katika mwaka huu wa fedha, halmashauri sita za Buchosa, Ilemela, Mwanza (Jiji), Magu, Sengerema na Ukerewe zimepokea takriban Sh bilioni 1.05 kwa ajili ya kujenga matundu ya vyoo 744, matangi ya maji 74 na miundombinu ya kunawia mikono 400.

Alisema serikali inaendelea kutoa fedha za ujenzi kupitia mpango wa Lipa Kutokana na Matokeo (EP4R), ambapo mkoa katika Mwaka wa Fedha wa 2020/21 ulipokea jumla ya Sh bilioni 1.6 kwa ajili ya ujenzi wa vyumba vya madarasa, matundu ya vyoo na mabweni kwa shule za sekondari.

"Shule za msingi zimepokea takribani Sh bilioni 2.92 kwa ajili ya ujenzi wa vyumba vya madarasa na matundu ya vyoo," aliongeza.

Akielezea mchanganuo wa fedha hizo kwa kila halmashauri, alisema halmashauri ya Buchosa ilipokea Sh milioni 466 zimetumika kujenga vyoo sita na madarasa mawili, Manispaa ya Ilemela- Sh milioni 195 kwa ajili ya vyoo-18 na bweni 1 na Halmashauri ya Kwimba Sh milioni 257,6 vyoo na madarasa-6 na mabweni-2.

Katika Halmashauri Misungwi ilipokea Sh milioni 120 kwa ajili y amadarasa mawili na bweni 1, Mwanza (Jiji) ilipokea takriban Sh milioni 520.9 zilizotumika kujenga vyoo 19 na madarasa 39, pamoja na Halmashauri ya Sengerema-takriban Sh milioni 136.6 kwa ajili ya vyoo 4, madarasa-4 na nyumba moja na wilaya ya Ukerewe ilyoipokea Sh 40,000,000/- ambazo imezitumia katika kujenga madarasa mawili.

# Gekul aagiza wakurugenzi kutenga asilimia 15 za mifugo, uvuvi

Na Mbaraka Kambona, Mwanga

NAIBU Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Pauline Gekul, amewataka wakurugenzi wa halmashauri nchini kutekeleza Waraka wa Mwaka 2002 unaowataka kutenga asilimia 15 ya mapato yanayotokana na shughuli za sekta ya mifugo na uvuvi na kuzirejesha katika sekta hizo ili kuboresha shughuli zake.

Gekul alitoa agizo hilo alipokuwa akizungumza na Viongozi wa Wilaya ya Mwanga, mkoani Kilimanjaro alipotembelea kukagua shughuli za sekta ya mifugo na uvuvi zinazotekelezwa wilayani humo juzi.

Kwa mujibu wa Gekul, mwaka 2002 serikali ilitoa waraka unaoelekeza halmashauri nchini kuhakikisha asilimia 15 ya mapato yanayotokana na shughuli za sekta ya mifugo na uvuvi, inatengwa na kurudishwa katika sekta kuboresha huduma kwa mifugo zikiwemo ukarabati wa majosho, minada na kununua chanjo za mifugo.

Alisema miundombinu mingi ya kuhudumia mifugo imechoka na akatolea mfano wa minada ya kuuzia ng'ombe akisema mingi haina uzio hivyo, mifugo inauzwa katika maeneo ya wazi jambo linalochangia upotevu wa mapato ya halmashauri.

"Najua katika halmashauri zetu, mara nyingi fedha huwa hazitoshi, lakini ni muhimu kujenga nidhamu ya matumizi ya fedha na tukifanya hivyo, itakuwa rahisi kutenga fedha hizo ili kuboresha sekta za mifugo na uvuvi, hivyo naagiza baada ya kutoka hapa tukatekeleze hilo," alisisitiza Gekul.

Aidha, Waziri Gekul alisema kuwa muelekeo wa serikali kwa sasa ni kuhakikisha majosho yanaboreshwa, minada inakarabatiwa na chanjo zinapatikana kwa urahisi ili wananchi washangaike kupata huduma kwa ajili ya mifugo yao.

# Wakurugenzi waagizwa kutenga fedha za mifugo

**Na Mbaraka Kambona,**
KILIMANJARO

NAIBU Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Pauline Gekul, amewataka wakurugenzi wa halmashauri zote nchini kutekeleza waraka wa mwaka 2002 unaowataka kutenga asilimia 15 ya mapato yanayotokana na shughuli za Sekta ya Mifugo na Uvuvi na kuzirejesha kwenye sekta hizo, ili kuboresha shughuli zake.

Alitoa agizo hilo alipokuwa akiongea na viongozi wa Wilaya ya Mwanga, mkoani Kilimanjaro alipotembelea kukagua shughuli za sekta hiyo zinazotekelezwa wilayani humo, Desemba 23, 2020.

Kwa mujibu wa Gekul, mwaka 2002 serikali ilitoa waraka ambao unaelekeza kuwa halmashauri zote nchini zihakikishe kuwa mapato yanayopatikana kutokana na shughuli za sekta ya mifugo na uvuvi itengwe asilimia 15 na zirudishwe kwa sekta hizo, ili kuboresha huduma kwa mifugo ikiwamo ukarabati wa majosho, minada na kununua chanjo za mifugo. "Wakurugenzi rejeeni huo waraka ambao unadumu mpaka mwaka 2025, ili mtekeleze kama ulivyoagiza na tukifanya hivyo itasaidia kuboresha huduma za mifugo yetu na tupate mazao bora yanayotokana na mifugo hiyo," alisema Gekul.

Vilevile, alisema miundombinu mingi ya kuhudumia mifugo imechoka akitoa mfano wa minada ya kuuzia ng'ombe kuwa mingi haina uzio, mifugo inauzwa katika maeneo ya wazi, jambo ambalo linachangia upotevu wa mapato ya halmashauri.

"Najua katika halmashauri zetu mara nyingi fedha huwa hazitoshi, lakini ni muhimu kujenga nidhamu ya matumizi ya fedha na tukifanya hivyo itakuwa rahisi kutenga hizo pesa ili kuboresha sekta za mifugo na uvuvi, hivyo naagiza baada ya kutoka hapa tukatekeleze hilo," alisisitiza Gekul.

Waziri Gekul alisema, mwelekeo wa serikali kwa sasa ni kuhakikisha majosho yanaboreshwa, minada inakarabatiwa na chanjo zinapatikana kwa urahisi, ili wananchi wasihangaike kupata huduma kwa ajili ya mifugo yao.

Pia, aliwataka maofisa mifugo kuhakikisha wanasimamia vyema ukusanyaji wa maduhuli ya serikali ili kuzuia upotevu wa mapato kwa kuwa makusanyo yakiwa mazuri na huduma za mifugo zitaboreshwa.

Scanned with CamScanner